

Maombi Wakati Umekata tamaa

Jarida la Maombi ya Wanawake Kimataifa



United Pentecostal Church

Agosti 2016



Imani Katikati ya Kukata tamaa

Na Liane Grant



Wakati mwingine watoto wetu kufanya mambo ambayo kutufanya kuomba sala la kukata tamaa. Moyo wa mama unahisi kuwa kama Mungu hataingilia, hali itakuwa mbaya kabisa, a kwa ajili yetu au yao.

Kukata tamaa ni hisia tete; inaweza kutuelekeza kuwa wenye na tumaini au bila . Tunapo omba ni laziwa tujue ya kuwa hatuwezi kuelekeza Mungu kuhusu majibu yake, kwa mfano "Mungu, lazima ufanyi hivi au tutaacha kukutumikia, utaacha kuwaombea watoto wetu na mengine kama hayo.

La ! Katika mambo yote, ni lazima tuombe mapenzi ya Mungu yatendeke. "Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia" (I Yohana 5:14). Mungu hajatuahidi kwamba hatutapata maumivu; wakati mwingine inahitajika ili tumurudie Mungu.Je, tuna imani ya kutosha ya kuomba kwa ajili ya mapenzi yake katika maisha ya watoto wetu, hata kama wanateseka ili kwa nafsi zao waokolewe?

Kukata tamaa kwetu hakulazimishi Mungu kujibu maombi.. Kwa zaidi ya miaka thelathini, niliomba kila siku kwa ajili ya uponyaji kutohana na matatizo ya kulala. Usiku kawaida, niliamka kama mara nane hadi kumi; na katika hoteli, ilikuwa zaidi ya mara arobaini au hamsini. Uchovu ilileta baadhi ya sala kukata tamaa, hasa wakati mimi nilikuwa natunza watoto wangu wandogo, kufanya kazi na kuwa mke wa mchungaji.

Niliamua nitakuwa kitandani kwa muda wa saa nane kila usiku, na mengine nikamwachia Mungu. Nilikataa kutawaliwa na shinda zangu. Mwaka jana, Mungu alimtuma mhubiri ambaye ni kijana kutoka mji mwingine kuniombea, na usiku huo kukawa na maendeleo ya ajabu. Baadaye,

mambo kuboreshwa hata zaidi wakati Mungu aliniongoza kwa chakula yenyе afya njema.

Mungu alijibu maombi yangu baada ya muda mrefu nilipojua nahitaji usaidizi kutoka kwa Mungu wa haraka, kwa sababu alijua ni kiasi gani ningeweza kuchukua, na kile nahitaji kujifunza kupertia hili jambo. "Kuna asiye na majoribu kuchukuliwa wewe lakini lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatakubali kujaribiwa juu mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu kufanya njia ya kutoroka, ili mpate kuwa kustahimili. " (I Wakorintho 10:13)

Nilipokuwa nikijiandaa kuandika makala hii, wimbo na Lauren Daigle alikuja kwenye redio: "Wakati huhamishi milima, mimi nina kuuliza utende; wakati wewe hautenganishi maji, natamani kupertia katikati ya maji; wakati hunijibu nakulilia wewe, nitatumaini, nitatumaini, mimi nitakutumainia ". Hebu tushikilia imani yetu tukiyaomba maombi haya.

Kumbuka: Liane na mumewe Scott wapanda kanisa katika Montreal-Quebec chini ya UPCI Metro Misheni mpango. Liane hutumika kama rais Quebec Ladies Ministries na ni mwanzilishi na msimamizi wa King's Translators, kundi la kujitolea kujitolea na kutoa rasilimali za kitume katika Ufaransa. Yeye kwa sasa anafanya utafiti wake na kundi hili tafsiri.

Swala la Kukata tamaa

Na Rebecca Akers



Hana hakuwa na watoto

Ilikuwa ni hofu ya wengi, lakini katika nyakati zake ilikuwa ni zaidi ya hofu. Ilikuwa ni mzigo - kitu yeye alikuwa akibeba. Alipoingia mlango wa kanisa (Hekalu) wamama wenzake walimuangalia kama hahitajiki kuwa huko.

Kila mahali aendapo, moto wa hukumu ulimchoma kupertia nyuma ya kichwa chake. Siku ilipita na yeye hakuwa na kula. hangeweza. Moyo wake ulikuwa mzungu mno na akili yake ilikuwa dhaifu mno. Mume wake alikuwa akimuuliza. "Kwa nini yeye hakuli? Kwa nini yeye analia? akamuuliza Je, si unanipend?" Lakini asingeweza kuhisi alivyokuwa akihisi.

Hili ikaiendelea kwa miaka mingi. Ilionekana kama mzunguko wenye maumivu na hamu.

Hanna akajawa na uchungu na hasira. *Kwa nini mimi Mungu? Kwa nini kunilaani na haya? Je, haunipendi mimi? Hauwezi kuona jinsi kila mtu ananidharau?*

Yeye akawa na uchovu.

Akakata tamaa.

Yeye aliomba sala ya kukata tamaa na aliapa kwamba kama Mungu atakapo mpa mtoto, atamrudishia amtumikie Hekaluni..

Hannna akamlilia Mungu bila kubakisha akiwa Hekaluni. Mpaka roho yake ilikuwa haikubakisha kitu na akakosa uwezo wa kuongea. Siku hiyo alipotoka hekalu "uso wake haukukunjamana tena."

Kufika mwisho ni silaha. Wakati wanaume na wanawake wa Mungu wanapofika, hakuna jambol linaloweza kuwasimamisha. Hasa wakati wao wakuomba. Maeneo mengi katika watu wa Biblia walimuomba Mungu kwa msaada, kwa amani, kwa ajili ya uongozi, kwa utupu wao kujazwa walipokuwa mapiganoni. Kama wewe uko kwa katika hali hii leo - umechoka, umefika mwisho - Mungu yuko tayari kukutana na wewe katika hali yako ya kukata tamaa.

Kumbuka: Rebecca ni msichana wa ajabu ambaye anapenda kumtumikia Mungu kwa moyo wake wote. Yeye ni mshiriki kamilifu katika wizara ya vijana, hufundisha shule ya Jumapili, kuimba katika kwaya, sifa timu na ina keyboard. Yeye pia hushiriki katika timu ishara,. Yeye niwa Baraza la Mwanafunzi na ni Makamu wa Rais wa sura shule yake ya National Honor. Katika muda wake vipuri yeye kujitolea katika hospitali kila wiki. Rebecca husaidia katika usambazaji wa jarida hili katika lugha mbalimbali. Mimi nina fahari kusema yeye ni mjukuu wangu! -Debbie Akers

Swala la Kufika Mwisho

Na Dianne Showalter



Maombi ya kufika mwisho ni maombi hakuna mtu ye yeyote mwenye hutuambia tusali, tunainamisha nyuso zetu, nakumsihi Mungu atuhurumie. Changamoto kubwa ni kujua jinsi ya kufanya hivyo ili maombi iwe na uzalishaj na kutuacha tukiwa huru wakati sisi tutakapo inuka kutokana na muda wetu pamoja na Mungu. (Soma Samweli 1: 7, 15; Samweli 2: 1.)

Moja ya yaliyo geuza maisha yangu ilikuwani wakati niliposikia misionari Nona Freeman akituambia kuhusu hali ya kufika mwisho wake kwa ajili ya wokovu wa wajukuu wake. Alilia kila siku akitaja majina yao katika maombi. Siku moja Mungu alimuuliza, "Je, unaamini mimi kwa hili?" Naye akasema, "Naam, Bwana." Kisha akasema, "Kama unaniamini, acha kunililia mimi na uanze kushereheke!" Ilikuwa wakati huo alipoanza kuinua picha zao juu kwa Mungu, na kutaja majina yao mbele zake, akisema, "Bwana, ninakushukuru kwa ajili ya kuokoa mjukuu wangu! Ni *itafanyika* katika jina la Yesu!" Hatimaye, wote wakaokolewa!

Wakati sisi tunapo ombo pamoja na watu ili wapokee Roho Mtakatifu, wakati mwingine tuna wahamasisha kumtukuza badala ya kuomba Mungu. Kutubu dhambi ni muhimu sana, lakini ni lazima tuendelee katika kwa kiwango cha juu zaidi ya msamaha. Tunaomba tunapotaka kwa machozi, lakini hatuhitaji kuishi hivyo kila siku. Ni lazima tuweke mizigo yetu miguuni mwake na kuanza kumtegemea na kutangaza neno lake tukiwa tumejawa na furaha, Yeye *anafanya* kazi!

Mwaka 1985 tulikuwa tumeitwa kuwa wamisenari El Salvador. Nilikuwa nataka, lakini nikawa na wasiwasii juu ya kuwapeleka watoto wangu katika nchi zenye vita. Katika mkutano wa wanawake nikasikia vile Hanna alipomchukua mtoto wake mdogo, Samuel, na akamuacha katika Hekaluni. Mimi nilikuwa karibu kuishi maumivu ya sadaka yake. Nililia kwa masaa mawili, na kisha nikasikia Bwana akiniambia, "Kama unataka kukaa na kutunza watoto wako mimi nitakukumbalisha, lakini kama wewe utakwenda, nami nitawatunza." Machozi yangu ikageuka kuwa shukrani na uaminifu, ukombozi na furaha! Mimi huamini maneno hayo mara nydingi, hata kama risasi iliingia ndani ya nyumba zetu, na Mungu amekuwa mwaminifu kwa neno lake!

Wakati binti yangu alikuwa amekabiliwa na maumivu kutokana na maumivu ya viungo. Nimlilia Bwana, "Kwa nini, Bwana? Yeye ana daima hukutumikia. Tuna imani kwa uponyaji wake. Je, unatusikia?" Katika hatua hiyo mimi akilini nikamchukua juu na kumlaza katika mikononi ya Yesu. Nikamwambia kwamba nilikuwa nampatia motto wangu ili afanye lolote ataye naye.. Ilikuwa ni vita ngumu, mzigo mzito kuinuliwa lakini imani ilianza. Alisikia kilio changu!

Kumbuka:

Dianne Showalter amefanya kazi karibu na mume wake kama mmisionari kwa miaka thelathini, alisafiri kwa mataifa zaidi ya 100, na anaongea katika mikutano ya wanawake mingi. Furaha yake ni kushiriki injilli hii ya thamani na kuwasaidia watu kuishi maisha ya ushindi kwake. Furaha yake kubwa ni kujua watoto wake wanaishi katika ukweli.

Kufika Mwisho!

Na Wanda Chavis



Kukata tamaa ni mahali pa kuwa bila matumaini na yasiyofumilika . Jinsi sisi huguswa na kukata tamaa inaweza leta kuheshimu au kutoheshimu Mungu.

Kwa miaka mingi, Hanna alikabiliwa na kukata tamaa yake kwa kulia, kununa, na huzuni. Unamkumbuka yeye? Mke Elkana?

"... Hana hakuwa na watoto" (I Samweli 1: 2, NKJV).

Hakuna maumivu kama kuwa mikono mitupu. Ilikuwa ni Hanna kila wakati - lakini kuna nyakati ambapo ukweli wa hali yake ilikuwa zaidi kuliko yeye anawenza kubeba. Wakati wao walienda Shilo kuabudu na kutoa sadaka ya familia zao, Elkana alikuwa akitoa sehemu ya familia kusherehekeea kukubaliwa na Mungu la sadaka zao za amani. Alihisi utupu na kukata tamaa, hata ingawa yeye alipewa heshima na Bwana yake. Wakati wa nyakati hizo, kuwaona watoto na mama yao, Penina, huku wakicheka na kula pamoja ilikuwa kama kuweka chumvi katika jeraha yake.

Mwaka baada ya mwaka angeweza kukataa kula, alikuwa akiaka hapo katika udhalilishaji, akiyafuta machozi . Hapo Penina akisherehekeea na kutoa maoni makali ili amuumize.

Mwaka baada ya Mwaka Hanna alikuwa akienda katika chumba cha kuombea na kumlilia Mungu, Kwa muda wa masaa manne Mumewe Elkana alijaribu kumsaidia lakini hakujuua amsaidie aje.

Mwaka huu Hanna hakuweza kwenda katika chumba cha maombi kumlilia Mungu na akajiangusha Hekaluni na kumlilia Mungu. Akamtolea Mungu moyo wake wote.

"Naye Eli, kuhani ameketi juu ya kitu na baada ya hekalu la Bwana. Na Hanna alikuwa katika uchungu wa roho, akamwomba Bwana, na kulia sana. Akaweka nadhiri, akasema, Ee Bwana wa majeshi , lakini kutega mimi mjakazi wako mtoto mume, ndipo mimi kumpa Bwana siku zote za maisha yake "(Samweli 1: 9-11).

Eli aliona sala yake ya kukata tamaa na walidhani yeye alikuwa amelewa; lakini baada ya kusikiliza, akampa baraka zake na alizungumza matumaini ndani ya moyo wake isiyo na matumaini!

Muendelezo wa hadithi hii ni wa ajabu , lakini nataka kumaliza mawazo yangu hapa.Unafanya nini na kukata tamaa kwaako? Kilio? Kulalamika? Nung'uniko?

Mimi changamoto yangu kwako nikumlilia Mungu, kumpatia maisha yako ya baadaye , na kufanya mipango yenyenye matumaini!

Kukata tamaa kwako ni fursa ya Mungu kwa matumaini na uponyaji. Usikufe moyo. Kuruhusu neno la Mungu kunena katika kila hali maishani mwako, uweke mipango yako kwa Mungu. Nadhiri. Naye atawapa furaha kwa huzuni. Vazi la sifa kufuta roho ya huzuni kubwa. (Soma Isaya 61.)

Kumbuka: Wanda Chavis mtumishi North Carolina District kama President wa Ladies Ministries na ni msemaji na mwandishi . Wanda pia anafanya kazi ya afya na taratibu mshauri wawanawake. Yeye ni mama fahari na 'MawMaw' kwa wajukuu wake.

Kutoka kwa Mhariri

Debbie Akers



Mungu anafanya mambo makuu

Mungu anafunga milango mingi na jarida hili ni sasa linapatikana kwa Kiingereza, Kihispania, Kifaransa, Kijerumani, Kiholanzi, Kireno, Kirusi, Kigiriki, Kiarabu, Kifarsi, Czech, Kichina, Kiswahili, Hungary, Kitagalogi, Indonesia Kirumi, Italiano na Norway. Tunaangalia kuongeza.Tafadhalii tusaidie na maombi kwa ajili ya mtafusiri wa Sebia, Bulgarian na Kijapan.

Kama unataka kupokea yoyote ya tafsiri hizi tafadhalii tuma ombi kwa (LadiesPrayerInternational@aol.com) na tutakuwa na furaha tele kuongeza wewe kwa orodha ya barua yetu!

Wizara

[Ladies Prayer International](#)
[UPCI Ladies Ministries](#)
[More to Life Bible Studies](#)
[Today's Christian Girl](#)
[World Network of Prayer](#)
[UPCI](#)
[My Hope Radio](#)
[Multicultural Ministries](#)



Sisi ni nani . . . Wanawake wa Maombi wa Kimataifa imeundwa na wanawake duniani kote tangu mwaka 1999. Wanawake hawa hukutana Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuungana katika maombi kwaajili ya watoto wao na watoto wa kanisa la mtaa na jamii.

Dhamira yetu . . . Nia yetu ni kuhifadhi kiroho kizazi hiki na zaidi, pia kurejesha kiroho vizazi vilivypita

Haja yetu . . . Wanawake watakaojiunga pamoja Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuombea watoto wao.

Vipaumbele vitatau vyta maombi...

1. Wokovu wa watoto wetu (Isaya 49:25; Zaburi 144:12, Isaya 43:5-6).
2. Kwamba wachukue umiliki wa imani katika umri wa kuwajibika (I Yohana 2:25-28; Yakobo 1:25).
3. Kwamba waingie katika huduma ya mavuno ya Bwana (Mathayo 9:38).

WIZARA TUNAZO SAIDIA

TUPELO CHILDREN'S MANSION

NEW BEGINNINGS

HAVEN OF HOPE

LIGHTHOUSE RANCH for BOYS



The Pure Path Series
from Tyndale Ministries

